TANGAZO LA SERIKALI Na. 724 la tarehe. 16/8/2024

SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI,
(SURA YA 297)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 109)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA EGONOMIA ZA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 288 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Egonomia za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Egonomia, ambazo katika Kanuni hizi zimerejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 2

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa kuongeza tafsiri ya msamiati ufuatayo:

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi;".

Marekebisho ya kanuni ya 3

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3-

(a) kwa kufuta neno "na" lililopo mwishoni mwa aya (a);

(b) kwa kuongeza aya ifuatayo mara baada ya aya (a):

"(b) mwajiriwa au mtu yeyote anayeweza kukumbwa na visababishi hatari vya egonomia; na";

(c) kwa kubadili mpangilio wa aya (b) kuwa aya (c).

Marekebisho ya kanuni ya 5

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa kufuta neno "za" lililopo kwenye maelezo ya pembeni na badala yake kuweka neno "vya".

Marekebisho ya kanuni ya

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 11 kwa kufuta na kuandika upya aya (b) kama ifuatavyo:

11 “(b) kwa kuzingatia masharti ya aya (c), wakati wa ukaguzi kuwasilisha kwa mkaguzi kumbukumbu za taarifa za afya zinazokusudiwa katika aya (a);”.

Dodoma
…………….., 2024

RIDHIWANI J. KIKWETE,
*Waziri wa Nchi,*
*Ofisi ya Waziri Mkuu,*
*(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)*